

*Shairi lifuatalo la Safari, limeandikwa na Mshairi Bakari Mwamboga wa Uholanzi, akizungumzia mauti, mazishi na yale yote yanayohusiana nayo, husasan anawakumbusha ndugu jamaa na marafiki kuwa kifo kipo kwa wote, na jambo la msingi ni kuomba duwa kwa Mwenyezi Mungu kufanya machungu ya siku hiyo kuwa mepesi kwa wale wanaobakia.*

## SAFARI

- |  |  |
|--|--|
| <p>1. Mola wangu yakarimu, naomba kwako jalali.<br/>Siku yangu ikitimu, nakuomba tafadhali.<br/>Yarabi isiwe ngumu, kwangu mimi na famili.<br/>Safari haiko mbali, kuelekea kuzimu.</p> <p>2. Yarabi Mola muumba, siku hiyo ikifika.<br/>Mola wangu nakuomba, wakifika malaika.<br/>Ni fumbue na kufimba, roho yangu ikitoka.<br/>Kwa wepesi ikitoka, ipepee kama pamba.</p> <p>3. Mola wangu siku hiyo, naomba Mola wanangu.<br/>Siku hii ya kiliyo, yakutoka roho yangu.<br/>Uzikaze zao nyoyo, wasome dua mafungu.<br/>Ukubali Bwana Mungu, mambo yote waombayo.</p> <p>4. Asilie mke wangu, siku hiyo ikifika.<br/>Sikitiko na uchungu, na mengine kadhalika.<br/>Ni mambo ya kilimwengu, wala si mja kutaka.<br/>Nyonda nikisha toweka, tutaonana kwa mungu.</p> <p>5. Mama nawe usilie, usilie wangu mama.<br/>Mama unihurumie, nendako nisende kwama.<br/>Mama sala nisalie, niombe dua njema.<br/>Mama nisamehe mama, mwana nisiangamie.</p> <p>6. Ndugu zangu kwa jumla, si nia niwakimbie.<br/>Wajibu hapa mahala, kila mtu apitie.<br/>Sote ni waja wa Mola, ndugu zangu msilie.<br/>Wanangu muangalie, yasiwapate madhila.</p> | <p>7. Marafiki ndugu zangu, tumeishi kwa imani.<br/>Munisamehe wenzangu, nilo kosa samahani.<br/>Leo ni safari yangu, nina kwenda kaburini.<br/>Marafiki maishani, na leo wazikwa wangu.</p> <p>8. Majirani mtakuja, musikose mazishini.<br/>Bakari si wa mmoja, naomba tafadhali.<br/>Munizike kwa pamoja, mtowe wenu huzuni.<br/>Mwenzenu ni safarini, safari ya kila mja.</p> <p>9. Wote wenzangu kazini, kifo changu waambiwe.<br/>Wasiwe na walakini, wajibu pia wajuwe.<br/>Roho mekwenda mbinguni, sirudi waarifiwe.<br/>Naomba kwenu isiwe, musiwawache gizani.</p> <p>10. Maiti yende nyumbani, maombi yangu mweyewe,<br/>Huko kwetu mashambani, kaburi nikachimbiwe,<br/>Na sala msikitini, halafu nikafukiwe,<br/>Namadeni nilipiwe, musiiwache kanuni.</p> <p>11. Mwisho nyote mshukuru, yangu mimi<br/>yamekwisha,<br/>Kaburini mukizuru, ndugu nina wakumbusha,<br/>Mola ametuamuru, kuniombea yatosha,<br/>Kulia kusiko kwisha, wenzangu mutanidhuru.</p> |
|--|--|

**B. Mwamboga**  
**Holland**  
**4.02.2003**

---